

Taarifa Kwa Vyombo vya Habari

**Madawa ya Kulevyta Nchini Tanzania na Mchango wake katika Mapato ya Kirasilitmali**

Vita dhidi ya madawa ya kulevyta vinaonekana kuzidi kasi nchini Tanzania baada ya Kamishna wa Eneo la Dar es Salaam kuamuru msururu wa ukamataji wa watu wenyewe haiba ya juu na maarufu. Vita hivi vilitiliwa nguvu zaidi na taarifa ya Rais kuwa vita hivi ni ajenda pana ambayo inapasa kujumuisha taasisi zote na uteuzi wake wa Kamishna Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Mihadarati (Taasisi ya Kutekeleza Udhhibit wa Madawa ya Kulevyta (DCEA)).

Kuhusiana na hili, sisi katika Hizb ut Tahrir Tanzania tunataka kuweka wazi yafuatayo:

1. Vita dhidi ya mihadarati nchini Tanzania vinaendeshwa kwa uhadaifu, kwani mfumo wa kirasilitmali unaotawala ulimwengu leo umejengwa juu ya msingi wa maslahi, ambapo kila kitu hupimwa kwa kipimo hicho. Zaidi ya hayo, siasa katika nidhamu ya kidemokrasia hufadhiliwa na warasilitmali amba mara nyingi huwa ni washikadau wakuu wa biashara ya madawa ya kulevyta. Hivyo ni wazi kuwa vita hivi dhidi ya madawa ya kulevyta vinakosa ikliasi, ni mwito mtupu wa kuwahadaa na kuwapurukusha watu kutokana na kufeli kwa serikali katika kadhia nyingi. Nyuma baadhi ya wanasiwa wenyewe vyeo vya juu walijigamba kuwa orodha ya wafanyi biashara wa madawa ya kulevyta iko mikononi mwao, ilhali licha ya mamlaka yao makubwa hawakusubutu kuwatata.
2. Nidhamu ya kidemokrasia inapiglia debe na kukuza fikra ovu na hatari ya 'uhuru wa kibinagsi' katika watu wake inayo washajiisha watu wengi kuingia katika matumizi ya mihadarati kama sehemu ya kufurahia uhuru wao. Hivyo basi, matumizi ya madawa ya kulevyta yana mahusiano ya moja kwa moja na fikra ya uhuru ambayo ndiyo fikra kuu katika demokrasia.
3. Mfumo wa kirasilitmali hususan nidhamu yake iliyo filisika ya kiuchumi imewatumbukiza wanadamu katika mateso mabaya ambayo yamewapelekea kupata msongo wa mawazo kutokana na athari yake ngumu na mbaya, mwishowe imewasukuma baadhi kudhani kuwa kujiingiza katika madawa ya kulevyta kutawaondolea mateso ya kiakili au hata kupata afueni ya muda. Urasilitmali unakosa suluhisho la kiroho la kumtuliza mwanadamu wakati wa shida.
4. Zaidi ya hayo, nidhamu ya kidemokrasia katika kuongeza maslahi ya kiuchumi inawasukuma watu kujisalimisha na kiasi kuwaabudu wasanii kama viigizo vyao vyema, amba baadhi yao ni watumizi wa madawa ya kulevyta. Natija yake vijana wengi waliopagawa wametumbukia ndani ya shimo la mihadarati.
5. Nidhamu ya kidemokrasia pamoja na mbinu yake ya kisekula katika sheria iliyo tungwa na wanadamu kamwe haiwezi kumaliza tatizo la madawa ya kulevyta, kutokana na tabia yake ya undumakuwili ya kuhalalisha baadhi ya aina za ulevi na kuharamisha nyingine. Huku kiuhalisia ikiwa aina zote za pombe zina madhara kwa wanadamu. Vipi utakuwa na ujasiri na maadili kupambana na madawa ya kulevyta, ilhali unaruhusu aina nyingine za madawa ya kulevyta?

Uislamu ndio mfumo pekee ulio na nguvu na imani na sheria kulinda mujtama kutokana na madawa ya kulevyta; na kukabiliana na vita hivi kikamilifu kuitia kupiga marufuku aina zote za ulevi. Wakati umewadia sasa hususan kwa wasiokuwa Waislamu kufurahia uadilifu wa Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah inayofanya kazi bila ya kuchoka kulinda hadhi ya wanadamu, mali, imani nk.

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

Simu: +255778 870609

Pepe: [mediarep@hizb.or.tz](mailto:mediarep@hizb.or.tz)

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)

Tovuti ya Hizb ut Tahrir Tanzania:

[www.hizb.or.tz](http://www.hizb.or.tz)

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.info](http://www.hizb-ut-tahrir.info)